1. UTANGULIZI

1.1 Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe

Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ni miongoni mwa Halmashauri 7 zinazounda Mkoa wa Mbeya ikiwa na ukubwa wa kilometa za mraba 1231.86. Kwa mujibu wa Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ilikuwa na Jumla ya watu 242,809 wakiwemo wanaume 115,510 na wanawake 127,299 ikiwa na kasi ya ukuaji wa idadi ya watu wa asilimia 2.7. Kwa mwaka 2019, Halmashauri inakadiriwa kuwa na Idadi ya watu ipatayo 302,430 (Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2019).

Uchumi wa Wilaya ya Rungwe hutegemea zaidi sekta ya kilimo hususani kilimo cha ndizi, parachichi, chai, kakao, kahawa, viazi mviringo, mahindi na mbogamboga na matunda ikiwa ni pamoja na mifugo ambavyo huajiri zaidi ya asilimia 80 ya wananchi wa Wilaya ya Rungwe. Shughuli nyingine hujumuisha utalii katika mlima Rungwe, maporomoko ya daraja la Mungu, Ziwa Ngosi ambalo ni ziwa litokanalo na Volkano, maporomoko ya maji ya Kaporogwe na kivutio cha Kijungu "pothole" kinachopatikana katika mto Kiwira miongoni mwa vivutio vingine. Pia, kuna shughuli za ufugaji wa nyuki, uhifadhi wa mazingira kupitia upandaji miti, biashara hususani za mazao ya kilimo na mifugo sanjari na bidhaa za viwandani, usafirishaji, madini hasa gesi asilia sanjari na uanzishwaji wa viwanda vidogo, vya kati na vikubwa ili kukuza uchumi wa kaya, kuongeza mapato ya Halmashauri na hatimaye kuboresha maisha ya mtanzania.

Pia, Halmashauri kwa kushirikiana na Serikali Kuu na wadau wa maendeleo imekuwa na jukumu la utoaji wa huduma za jamii ikiwemo elimu, afya, maji, na miundombinu ya barabara na masoko kwa kushirikiana na wananchi ambao wamekuwa wakishiriki kikamilifu katika utekelezaji wa miradi mbalimbali inayolenga kutoa huduma bora zenye ufanisi na tija kwa jamii.

2. MAFANIKIO YA WILAYA YA RUNGWE KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 5 YA SERIKALI YA AWAMU YA TANO (2015 – 2020)

Tangu Serikali ya awamu ya tano ilipoingia madarakani mwaka 2015, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe imefanikiwa kufanya yafuatayo ambayo yamepelekea kuendelea kuboreka kwa maisha ya wananchi wa Rungwe na Tanzania kwa ujumla;-

2.1 Sekta ya Elimu

Elimu ni nyenzo ya ukombozi katika nyanja za kijamii, kiuchumi na utawala bora. Katika kipindi cha miaka 5 ya awamu ya tano, Halmashauri imefanikiwa kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia ikiwa ni pamoja na ujenzi wa shule mpya ya Sekondari 3, ujenzi wa mabweni katika Shule za Sekondari Bulyaga, Masoko, Ikuti, na ujenzi na ukarabati wa maboma ya vyumba vya madarasa 33 ambapo maboma 25 ni kwa shule za msingi na

maboma 8 kwa shule za sekondari.Miradi hii imetekelezwa kupitia fedha za P4R (lipa kwa matokeo) ambapo hadi kufikia mwezi Julai 2020, jumla ya maboma 30 yamekamilika na yanatumika ambapo kiasi cha sh. **412,500.000.00** kilitolewa na serikali kuu kupitia mradi wa P4R. Aidha, kiasi cha sh. **1,307,302,202.00** kimetolewa na serikali kuu kupita mradi wa EP4R kukamilisha ujenzi wa vymba vya madarasa 22 na ukarabati mkubwa wa shule kongwe ya Rungwe ambao unaendelea kwa sasa. Jedwali Namba 1 linaonesha mafanikio katika sekta ya Elimu kwa kipindi miaka mitana kinachoanzia mwaka 20215/2016 hadi 2019/2020.

	SEKTA	**SHUGHULI**	**ILIVYOKUWA 2015**	**ILIVYO SASA 2020**	**MAELEZO**
1.	**Elimu Msingi**	Idadi ya shule za Serikali	139	142	Shule 3 mpya zimefunguliwa- ongezeko la 3%
		Idadi ya shule binafsi	3	5	Shule 2 zimefunguliwa
		Madarasa yaliyojengwa	852	954	Madarasa 102 yamejengwa- ongezeko la 11%
		Idadi ya matundu ya vyoo	1,101	1,828	Matundu 727 yamejengwa- ongezeko la 66%
		Nyumba za walimu	259	294	Nyumba za walimu 35 zimejengwa sawa na ongezeko la 13%
		Idadi ya madawati	14,174	18587	Madawati 4,413 yametengenezwa
		Kiwango cha ufaulu kwa Wanafunzi darasa la IV na VII	3,694	5,451	Ufaulu umeongezeka kwa 47%
		Fedha iliyotolewa kwa ajili ya Elimu bure.	34,496,000	311,134,075	Fedha zaaelimu bure zimeongezeka kwa 11%
		Fedha iliyotolewa kwa ajili ya posho ya madaraka.	0	425,400,000	-
2.	**Elimu Sekondari**	Idadi ya Shule za Serikali	28	32	Shule 4 zimeongezeka
		Idadi ya Shule	8	10	Shule 2 zimeongezeka

		binafsi			
		Madarasa yaliyojengwa.	328	454	Madarasa 126 zimeongezeka kwa 38%
		Idadi ya matundu ya vyoo	595	927	Matundu 332 zimeongezeka kwa 55%
		Nyumba za waalimu	92	100	Nyumba 8 zimejengwa 8%
		Idadi ya madawati	14,312	19,118	Madawati ,4806 yametengenezwa
		Kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi kidato cha II,IV na VI	II 93 %	95%	Ufaulu umeongeza
			IV 72.53 %	89.14%	Ufaulu umeongeza
			VI 92 %	99%	Ufaulu umeongeza
		Idadi ya vyumba vya maabara	84	88	Maabara 4 zimejengwa sawa na ongezeko la 4.7%
		Fedha iliyotolewa kwa ajili ya posho ya madaraka.	84,000,000.00	90,000,000.00	Posho za madaraka zimeongezeka kwa sababu ya shule kuongezeka. (7%)

2.2 Sekta ya Afya

Sekta ya afya ni miongoni mwa sekta muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla. Kwa kuzingatia hilo, Serikali ya awamu ya tano imekuwa ikielekeza rasilimali fedha na watu katika kuhakikisha kuwa huduma za afya zinatolewa kwa ufanisi na tija kupitia ujenzi na ukarabati wa Hospitali, vituo vya afya na zahanati. Kwa kipindi cha miaka 5 ya Serikali ya awamu ya tano, Halmashauri imefanikiwa kujenga na kukarabati jumla ya vituo vya afya vitatu (3) ambavyo ni kituo cha afya cha Masukulu, Ikuti na Isongole na kituo cha afya cha Mpuguso ambacho kinaendelea kujengwa. Pia, Halmashauri inaendelea na uboreshaji wa mazingira ya kutolea huduma ya afya kupitia ujenzi wa wodi ya mama na mtoto ya Hospitali ya Wilaya ya Rungwe-Makandana, ujenzi wa zahanati ya Isyonje na nyinginezo. Aidha uhamasishaji wa jamii unaendelea ili kutekeleza mpango wa kujenga Zahanati kila Kijiji na kituo cha Afya kila Kata na kinatarajia kuanza kutoa huduma mwishoni mwamwezi Agosti. Jedwali Namba 2 linaonesha mafanikio katika sekta ya Afya kwa kipindi miaka mitano kinachoanzia mwaka 20215/2016 hadi 2019/2020.

	SEKTA	SHUGHULI	ILIVYOKUWA 2015	ILIVYOSASA 2020	MAELEZO
3.	Afya	Idadi ya Zahanati za Serikali	34	36	Zahanati 2 zimejengwa na kukamilika (Ongezeko la 5.8%)
		Idadi ya Zahanati binafsi	4	5	Zahanati 1 imeongezeka (Ongezeko la 25%)
		Idadi ya vituo vya afya vya Serikali	2	3	KItuo kimoja kimejengwa (Ongezeko la 50%)
		Idadi ya vituo vya afya binafsi	2	2	Hakuna kituo binafsi kilichoongeza
		Hospitali za Wilaya	1	1	Hakuna Hospitali iliyoongezeka
		Hospitali binafsi	1	1	Hakuna Hospitali iliyoongezeka
		Zahanati, vituo vya afya na hospitali vilivyofanyiwa ukarabati	-	3	Vituo vitatu vimekarabatiwa
		Nyumba za watumishi zilizojengwa/zilizo karabatiwa.	96	99	Nyumba tatu mpya zimejengwa
		Idadi ya wanaufaika ICHF	-	8565	
		Idadi ya wazee waliotambuliwa na kupewa vitambulisho	4,500	6,710	Wazee 2,210 wametambuliwa zaidi ya waliokuwepo mwaka 2015 (Ongezeko la 49%)

2.3 Sekta ya Maji

Katika kipindi chote cha kuanzia mwaka 2015 hadi 2020 Serikali imekuwa ikitekeleza shughuli mbalimbali Kwa ajili ya kuwaletea wananchi maendeleo kama ilivyoelekezwa katika Ilani ya Uchaguzi mkuu ya CCM ya mwaka 2015. Serikali katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe imekuwa ikitekeleza shughuli na miradi mbalimbali kama zilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya mwaka 2015.

Katika kipindi hiki Serikali imetekeleza shughuli mbalimbali kupitia sekta ya maji kama ifuatavyo:

	SEKTA	SHUGHULI	ILIVYOKUWA 2015	ILIVYO MWAKA 2020	MAELEZO
4.	Maji	Upatikanaji wa huduma ya maji	58.7%	73.1%	Ongezeko la 14%
		Ukarabati na upanuzi wa miradi ya maji	Miradi 22	Miradi 36	Ongezeko la miradi 14 sawa na 61%
		Uanzishwaji wa Jumuiya za watumiaji maji	Jumuiya 10	Jumuiya 38	Ongezeko la jumuiya 28 sawa na 26%
		Kuhifadhi vyanzo vya maji	Vyanzo 22	Vyanzo 56	Ongezeko la vyanzo 34 sawa na 39%

2.4 Sekta ya Viwanda, Biashara na Masoko

Hii ni miongoni mwa sekta ambazo zimekuwa zikipewa msukumo mkubwa sana kupitia Serikali ya awamu ya tano. Hii ni kwa sababu viwanda husaidia katika kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi, maji, madini na misitu ikiwa ni pamoja na kutengeneza fursa za ajira na masoko kwa wananchi. Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe haipo nyuma katika utekelezaji wa azma hii ya Serikali ya awamu ya Tano katika kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda. Jedwali Namba 3 linaonesha mafanikio katika sekta ya viwanda na Biashara kwa kipindi cha miaka mitano kinachoanzia mwaka 20215/2016 hadi 2019/2020

Aidha, uwepo wa viwanda hivi imesaidia kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa Wilayani Rungwe ikiwa ni pamoja na kuongeza wigo wa ajira na mapato ya Halmashauri. Miongoni mwa viwanda hivi ni pamoja na viwanda vya kuchakata chai (WATCO), viwanda vya kuchakata parachichi (KUZA, Rungwe Avocado Company na Mohamed Enterprise). Pia, Halmashauri imeendelea kuboresha miundombinu ya masoko ikiwemo soko kuu la Tukuyu, Soko la ndizi Tandale, soko la Kiwira, Machinga na Garden na sasa inaendelea na uboreshaji wa miundombinu ya masoko ya Mpuguso na Mwambenja ili kuwa na mazingira bora ya kufanyia biashara yanayojali afya za watumiaji wa bidhaa na tija kwa wafanyabiashara.

SEKTA	SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA.	HALI ILIVYOKUWA 2015/2016	HALI ILIVYO 2020	MAELEZO
5. Viwanda na biashara	Viwanda vikubwa vilivyoanzishwa	03	03	Hakuna kiwanda kikubwa kilichojengwa
	Viwanda vya kati vilivyoanzishwa	02	06	Ongezeko la

				viwanda 04
	Viwanda vidogo vilivyoanzishwa	68	111	Ongezeko la viwanda vidogo 43
	Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya viwanda (idadi na ukubwa)	00	Ekari 26 - Kyimo Ekari 100 – Ilenge	Jumla ya Ekari 126

2.5 Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani

Ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri umekuwa pia ukiongezeka mwaka hadi mwaka tangu Serikali ya awamu ya tano ilipoingia madarakani kunakotokana na kuzuiwa kwa mianya ya upotevu wa mapato na utumiaji wa mashine za kielektroniki ambazo zimeongeza ufanisi na tija katika ukusanyaji wa mapato licha ya changamoto zitokanazo na teknolojia hii. Uwezo wa Halmashauri kujitegemea katika bajeti zake umekuwa ukiongezeka kutoka 6.9% mwaka 2016/17 hadi kufikia 9.7% mwaka 2019/20. Jedwali Namba 4 linaonesha hali ya ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kipindi miaka mitano kinachoanzia mwaka 2015/2016 hadi 2019/2020

Hali ya ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri kuanzia mwaka wa Fedha 2015/2016 hadi 2019/2020

MWAKA	**KIASI KILICHPANGWA**	**KIASI KILICHOKUSANYWA**	**ASILIMIA**
2015/2016	2,652,275,330.00	2,542,022,270.00	93
2016/2017	3,714,743,750.00	3,627,797,221.00	98
2017/2018	3,992,665,270.00	3,414,723,367.67	86
2018/2019	3,183,208,440.00	2,954,656,100.62	92
2019/2020	5,371,119,322.00	4,425,164,812.21	82.4
JUMLA	**18,914,012,112**	**16,964,363,771.5**	**90.28**

2.6 Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Uwezeshaji wa wananchi kiuchumi umekuwa ukifanyika kupitia kuwajengea uwezo wananchi kuhusu ujasiriamali, biashara na kujitegemea kwa kuwahamasisha wananchi hususani vijana, akina mama na watu wenye ulemavu kujiunga katika vikundi na kuvisajili na hatimaye kupewa mitaji ya uanzishwaji wa shughuli za kiuchumi kupitia mikopo inayotolewa na Halmashauri. Kiwango cha mikopo kimeongezeka kutoka Tsh 95,898,120.70 mwaka 2015 hadi kufikia Tsh 483,000,000.00 kwa jumla vikundi 87 ambapo Wanawake vikundi 56, vikundi vya Vijana 28 na vikundi 3 vya Watu Wenye Ulemavu mwaka 2019/2020 Vikundi hivi hujishusisha na shughuli za uzalishaji mali

ikiwemo shughuli za kilimo, ufugaji na baadhi wameanzisha viwanda vidogo vidogo vya kusindika mazao ya kilimo na vyakula vya mifugo.

	SEKTA	SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA	HALI ILIVYOKUWA 2015/2016	HALI ILIVYO 2020
6	Maendeleo ya Jamii	Thamani ya mikopo iliyotolewa kwa vikundi	2,000,000.00	483,000,000
		Mikopo kwa wanawake	0.00	281,000,000.00
		Mikopo kwa vijana	2,000,000.00	189,500,000.00
		Mikopo kwa walemavu	0.00	12,500,000.00
		Idadi ya vikundi vilivyosajiliwa	41	214
		Idadi ya kaya maskini zilizotambuliwa	3,802	3,668
		Idadi ya kaya maskini zilizonufaika	3,801	3,627

2.7 Miundombinu ya Barabara

Usafiri kwa njia ya barabara Wilayani ni wa kuridhisha na umekuwa ukiboreka kila mwaka isipokuwa kwa sehemu chache zenye utelezi ambapo barabara ni za udongo mtupu bila changarawe. Kwa mwaka 2015/2016, wakati Serikali ya awamu ya tano inaingia madarakani, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ilikuwa na mtandao wa barabara wenye jumla ya Kilomita 725.93. Kati ya hizo, Kilomita 2.9 ni barabara ya lami, kilomita 154.43 ni barabara za Changalawe, na kilomita 568.6 ni barabara za udongo. Kwa kipindi cha miaka 5 ya uongozi wa awamu ya tano, barabara zimeendelea kutengenezwa na kukarabatiwa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa madaraja matatu uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2018/19 na matengenezo yamekuwa yakifanyika mara kwa mara.

2.8 Sekta ya Kilimo na Ushirika

Kwa ujumla, Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe inajitosheleza kwa chakula na ziada huuzwa katika mikoa na nchi jirani za Malawi na Zambia. Kupitia mikakati thabiti ya kukifanya kilimo na mifugo kuwa cha kibiashara badala ya kilimo na ufugaji wa kujikimu, uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo umekuwa ukiongezeka kila mwaka licha ya wakati mwingine kushuka kutegemea hali ya hewa. Hii imetokana na uwepo wa huduma za ugani karibu zaidi na wananchi kupitia msisitizo na maelekezo ya uongozi wa awamu ya tano unaowataka maafisa ugani kuwatembelea wakulima na wafugaji na kutoa ushauri wa kitaalamu badala ya kutumia muda mwingi ofisini kama ilivyozoeleka.

	SEKTA	SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA	HALI ILIVYOKUWA 2015/2016			HALI ILIVYO 2020	MAELEZO
6	**Kilimo**		Na.	Zao	Kiasi	Kiasi	
			1	Mahindi	Tani 103,737	Tani 103,990	Uzalishaji umeongezeka kwa 24.34%
			2	Mpunga	Tani 3,023.0	Tani 2,995	Wakulima kuhamia katika mazao mengine na maeneo mengi kupandwa parachichi.
			4	Mihogo	111,455	120,505.50	Uzalishaji umeongezeka kwa 8%
			5	Gimbi	7,820	88,730.10	Uzalishaji umeongezeka kwa 1,034%
			6	Viazi mviringo	503,119.0	504,060	Uzalishaji umeongezeka kwa 0.18%
			8	Ndizi	356,404.0	475,273	Uzalishaji umeongezeka
		Kiwango cha uzalishaji wa mazao ya biashara	1				
			2				
			3	Kahawa	291.6	648	Uzalishaji umeongezeka kwa 122%
			4	Chai	7,877.8	7,969.5	Uzalishaji umeongezeka kwa 1.1%
		Pembejeo zilizopokelewa	Mbolea				
			13,572.8 (Tani)			12,960(Tani)	Zimeshuka kutokanana kuondole kwa ruzuku ya pembejeo.
		Viuatilifu (Madawa ya mimea)	15,211.4 (lita)			28,132	Uzalishaji umeongezeka kwa 45.92%
		Idadi ya watumishi	100			73	-
		Vituo vya rasilimali za kilimo	1			1	-

		Idadi ya SACCOS	37	31	SACCOSS 06 zimefutwa kutokana na kutofanya kazi kwa muda mrefu
		Idadi ya AMCOS	17	50	Ongezeko la 66%
		Mbegu	240	268.2	Ongezeko la 89.4%

2.9 Sekta ya Mifugo.

Sekta ya mifugo uchangia kiasi kikubwa cha uboreshaji wa maisha ya wakazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe. Katika serikali ya awamu ya tano shughuli mbalmbali zimefanyika katika utekelezaji wa sera ya mifugo ya Taifa inayolenga kuboesha ufugaji wenye tija kwa wananchi na kuongeza mnyororo wa thamani wa mifugo**.** Jedwali hapa chini linaonesha shughuli zilizotekelezwa katika kipindi cha miaka mitano ya serikali ya awamu ya tano kinachoanzia mwaka 2015/2016 hadi 2019/2020.

	SEKTA	**SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA**	**HALI ILIVYOKUWA 2015/2016**		**2019/2020**	**MAELEZO**
8	**Mifugo**	Idadi ya mifugo (taja kwa kila aina)				
			Ngombe wa Kisasa	27,957	40,820	Ufugaji umeongezeka kwa 64.4%
			Mbuzi wa asili	2,013	7,830	Ongezeko la 25.71%
		Idadi ya majosho yaliyokarabatiwa		0	2	-
		Idadi ya ng'ombe waliopatikana kwenye uhimilishaji		288	532	Ng'ombe wameongezeka kwa 54%
		Kiwango cha ngozi kilichozalishwa		10,183	8,091	Soko la ngozi lilishuka kwa miaka 03 kwa sasa linaendelea vizuri na asilimia 85 zinanunuliwa
		Vituo vya kukusanyia Maziwa		01	12	Lengo lilikuwa kuwa na vituo 10 sawa na ongezeko la 110%

9.	**Uvuvi**	Kiwango cha uzalishaji wa samaki na dagaa	1,401	4,029	Ongezeko la 34.77%
		Idadi ya mabwawa yaliyojengwa	250	296	Ongezeko la 84.44%
		Kiwango cha uzalishaji wa samaki na dagaa	1,401	4,029	Ongezeko la 34.77%

2.10 Sekta ya Utawala

Shughuli ya kusimamia utawala bora katika ngazi ya Halmashauri ikiwa ni pamoja na kufanikisha usimamizi wa vikao ngazi ya vijiji na Kata, usimamizi majukumu na haki za watumishi kwa kuzingatia sheria, taratibu na miongozo mbalimbali imeweza kutekelezwa kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2015/2016 hadi 2019/2020 kama inavyoonekana hapa chini;

	SEKTA	**SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA**	**HALI ILIVYOKUWA 2015/2016**	**HALI ILIVYO 2020**	**MAELEZO**
10	**Utawala**	Idadi ya Ofisi za Kata	06	10	Ongezeko la 48.2%
		Idadi ya Ofisi za Vijiji	60	125	Ongezeko la 81%
		Idadi ya watumishi waliopata mafunzo (ya muda mrefu na muda mfupi)	65	399	Ongezeko la 95%
		Vikao vilivyofanyika kwa ngazi ya msingi.	1,491	7,580	Ongezeko la 80%

2.11 Sekta ya Ardhi

Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ina jumla ya Hekari 123,186 kati ya hizo hekari 83,613.6 zinafaa kwa shughuli za uzalishaji wa mazao ya kilimo na hekari 39,572.4 sawa na asilimia 32 ina milima, mabonde, misitu, mito na maeneo ya makazi. Ili matumizi ya ardhi yanakuwa endelevu, katika kipindi cha miaka mitano ya awamu ya tano, shughuli zifuatazo zimefanyika katika kuhakikisha sekta ya ardhi inaboresha maisha ya wananchi, shughuli zifuatazo zimefanyika;

SEKTA	SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA	HALI ILIVYOKUWA 2015/2016	HALI ILIVYO 2020	MAELEZO
11.Ardhi	Kuongeza idadi ya hatimiliki za viwanja	36	240	Ongezeko la 85%
	Kuongeza idadi ya hatimiliki za kimila	1018	1893	Ongezeko la 53%
	Kuongeza idadi ya Vijiji vilivyoandaliwa matumizi bora ya ardhi	121	125	Ongezeko la 99.2%
	Kuongeza idadi ya viwanja vya makazi vilivyopimwa	34	701	Ongezeko la 95.14%
	Kuongeza idadi ya hatimiliki za viwanja	36	240	Ongezeko la 85%

Pamoja na muhtasari huu nimeambatanisha na jedwali linaloonesha miradi na shughuli zilizotekelezwa katika kipindi cha miaka mitano.

LOEMA I. PETER

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

RUNGWE